# SHULE BORA

Elimu bora kwa watoto wote

MUHTASARI WA

# RIPOTI YA MWEZI

Septemba 2022



**Mwezi Septemba Shule Bora imeendelea kujenga misingi imara ya utoaji wa elimu bora, salama na jumuishi kote nchini Tanzania. Ushirikiano na kubuni kwa pamoja na serikali na taasisi wabia vinaendelea kuimarika, huku Shule Bora ikitoa utaalamu na msaada kwa maendeleo ya walimu na elimu ya awali, na kuisaidia serikali kuwafikia wanajamii na kuwashirikisha. Mfululizo wa tafiti msingi unajenga ushahidi wa utekelezaji, ambapo matokeo ya Mpango wa Elimu wa Lipa Kulingana na Matokeo (EPforR) yanaonesha kuwa kuna ishara nyingi zinazoleta matumaini.**



*Mpango wa Elimu wa Lipa Kulingana na Matokeo (EPforR) ni programu bunifu ya kuboresha mifumo inayotekelezwa kitaifa, ikigharamiwa na wafadhili wa kimataifa ambao ni pamoja na UK Aid. Mpango huu uliundwa ili kuhamasisha na kukuza motisha ya upatikanaji sawa wa elimu bora kwa ngazi ya elimu ya awali na msingi nchini Tanzania. Kupitia kutoa msaada wake wa kiuftaalamu, EPforR inawezesha upatikanaji wa ushahidi, uandaaji wa mipango na ugawaji wa rasilimali ili, kwa kufikia malengo na vigezo vinavyohusiana na matokeo ya utekelezaji wa kisekta, Serikali ya Tanzania itahakikisha fedha nyingi zaidi zinatolewa kwenye mfumo wa elimu.*

## Uimarishaji wa Mfumo wa Mpango wa Elimu wa Lipa Kulingana na Matokeo (EPforR) Unatoa Matokeo ya Kuvutia

Mpango wa Elimu wa Lipa Kulingana na Matokeo (EPforR) umebuniwa ili kuleta matokeo makubwa na endelevu katika elimu kwa kusaidia kuanzisha na kuimarisha mifumo na taratibu za elimu. Na kwa kufanya hivyo, kuleta maboresho mahususi muhimu kwenye matokeo ya kujifunza, hasa kwenye stadi za kusoma, kuandika na kuhesabu, na kuhakikisha watoto wengi zaidi wanaendelea kujifunza na kuhitimu elimu ya msingi, kunakojulikana kama kiwango cha kubaki shuleni hadi kuhitimu elimu ya msingi. Mwezi Septemba, mchakato wa uhakiki wa Mpango wa Elimu wa Lipa Kulingana na Matokeo (EPforR 2021/22) ulikamilika, na mpango huo umepata wastani wa matokeo ya utekelezaji wa mwaka ni takribani 90%. Asilimia hizi zinalinganishwa na kiwango cha asilimia za miaka saba iliyopita, ambayo ilionesha utekelezaji wa wastani wa 79.4%. Mwaka huu, Halmashauri 98 ziliboresha au kudumisha viwango vyao vya wanafunzi kubaki shuleni hadi kuhitimu elimu ya msingi. Maboresho mengine makubwa ni pamoja na kupanda kwa ufaulu katika stadi za Kusoma kwa Ufahamu, ambao ilionesha ongezeko la 7%, stadi za kuhesabu iliboreka kwa 16% na Fahirisi ya Usawa wa Jinsia inayoonesha ufaulu na kuendelea na masomo, inaonyesha upatikanaji wa elimu kwa wasichana na wavulana,umeongezeka kutoka 99.1% hadi 100.01%.

## Kujenga Timu ya Mabingwa wa Mawasiliano katika Halmashauri

Msingi wa mbinu ya Shule Bora ni kuhakikisha Serikali inaongoza, inakuza umiliki wa pamoja, ushirikiano, na mipango ya pamoja katika ngazi zote. Kujenga uwezo wa serikali za mitaa wa kuwasiliana, kutangaza kazi zao na kuwafikia wazazi na jamii ni muhimu katika harakati za kuboresha matokeo ya ujifunzaji. Mwezi Septemba, Maafisa Habari wa ngazi za Kitaifa, Mikoa na Halmashauri walipatiwa mafunzo yaliyohusu mbinu bora na mahiri za mawasiliano, ikiwemo kuandika kwa ufanisi, kuwasilisha mada, kutumia simu za kisasa kupiga picha na video zenye ubora wa hali ya juu na kutengeneza maudhui ya kuvutia kwenye vyombo vya Habari na kwenye mitandao ya kijamii. Mafunzo hayo yalihusisha Maafisa Habari kutoka kwenye Halmashauri zote za Mikoa tisa inayotekeleza Mpango wa Shule Bora. Mafunzo haya ni sehemu ya mbinu ya uimarishaji mifumo ya Shule Bora inayolenga kuimarisha utoaji wa elimu bora ya msingi nchini Tanzania. Zaidi ya washiriki sabini kutoka mikoa ya Mara, Simiyu, Singida,Tanga, Pwani na Dodoma walinufaika na washiriki wengine wataendelea kunufaika kwa kupatiwa mafunzo mwezi Oktoba. Ingawa kuna mengi ya kufanya ili kujenga uwezo wa mawasiliano ya ndani, mafunzo haya yanaonekana kuwa yameanzisha jukwaa imara la mawasiliano na uhamasishaji kwa niaba ya Shule Bora.

## Jumuiya za Kujifunza Kusaidia katika Maendeleo ya Kitaaluma ya Waalimu

Serikali ya Tanzania imedhamiria kujenga nguvukazi ya kisasa, yenye walimu wenye uwezo wa hali ya juu na wenye weledi ambao wana jukumu kubwa katika kufikia matarajio ya maendeleo ya taifa. Shule Bora inatoa msaada mkubwa kwa maendeleo ya walimu, ikifanya kazi kwa kushirikiana na Serikali na Taasisi ya Elimu Tanzania (TIE) katika kutekeleza sera ya maendeleo endelevu ya kitaaluma ya walimu nchini (TCPD). Ushahidi wa kimataifa unaonesha kuwa kuwaleta walimu pamoja katika Jumuiya za Kujifunzaji ili kutatua changamoto za darasani kwa pamoja katika ngazi ya jamii ni mojawapo ya mipango madhubuti zaidi ya kuboresha ufundishaji na ujifunzaji, na sera ya maendeleo endelevu ya kitaaluma ya walimu nchini inachochea mbinu za ugatuzi za gharama nafuu katika ngazi za kikanda. Hadi kufikia mwisho wa mwezi Septemba Shule Bora, kwa kushirikiana na TIE, Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia na TAMISEMI, walikuwa wameanzisha mafunzo elekezi juu ya sera ya maendeleo endelevu ya kitaaluma ya walimu nchini kwa Maafisa Elimu Kata 352 (AEK), viongozi wa elimu wa Halmashauri 428, walimu wakuu 1500, walimu wa taaluma 1500 na walimu wawezeshaji rika 1500 ya kuanzisha Jumuiya za Kujifunza ambazo zitatumia Mfumo wa Usimamizi wa Ujifunzaji (LMS), kama chombo cha kuchochea ubora kwenye ufundishaji na ujifunzaji.

## Kujenga Misingi Imara ya Ujifunzaji

Kuwatayarisha watoto kujifunza wanapoanza shule ya msingi kunaaminika kuwa na mchango mkubwa katika kuboresha matokeo ya ujifunzaji. Shule Bora inawekeza katika kuisaidia Serikali ya Tanzania kutengeneza Mpango wa kumuandaa Mtoto Kuanza Shule (SRP) kwenye mikoa tisa iliyochaguliwa, kwa kuendeleza mafanikio ya awali ya EQUIP-T, programu iliyotekelezwa mwaka 2014-2019 kwa ufadhili wa Serikali ya Uingereza kupitia FCDO.

Mwezi Septemba, Shule Bora imetoa mafunzo kwa maafisa elimu na walimu kutoka Shule Mama, ambazo zinafanya kazi kama vituo walezi wa Vituo vya Utayari katika kata kumi na nne za majaribio katika mikoa ya Simiyu na Rukwa. Mafunzo hayo yaliandaliwa ili kuwaelekeza wadau kuhusu majukumu na wajibu wao wa kuanzisha na kuendesha vituo vya Elimu ya Utayari. Aidha, walimu 37 wa kujitolea kutoka kwenye jamii walipatiwa mafunzo kwa muda wa siku 5 kuhusu majukumu na wajibu wao kwenye mbinu bora za ufundishaji na ujifunzaji katika Vituo vya Utayari. Halmashauri za Wilaya za Rukwa na Simiyu sasa zimeanzisha Vituo 41 vya Shule za Utayari (17 Rukwa na 24 mkoani Simiyu), kila kituo kina wafanyakazi na kimepatiwa vifaa mbalimbali vya kufundishia na kujifunzia. Mkoa wa Rukwa tayari umeandikisha watoto 1,359 (wavulana 710 na wasichana 649) katika vituo vya madarasa ya utayari na mkoa wa Simiyu umeandikisha watoto 747 (wavulana 360 na Wasichana 387) ambao watajiunga kwenye Vituo 41 vya Utayari mwezi ujao. Mafunzo kwa mkoa wa Pwani yatafanyika mwezi Oktoba.

## Kujenga Msingi wa Ushahidi kwa ajili ya Utekelezaji wa Programu kwa Mafanikio

Shule Bora na wabia wake serikalini wamejidhatiti kuweka msingi thabiti wa ushahidi kwa ajili ya programu wanazobuni na kuzitekeleza ili kuweka msingi imara zaidi wa mafanikio na kupanua wigo wa maeneo ya utekelezaji. Hii ina maana kuweka misingi halisi, kutambua na kujifunza kutokana na mambo ambayo yalifanikiwa hapo awali, kujumuisha taarifa kutoka vyanzo mbalimbali, na kutengeneza njia bora za ufuatiliaji na tathmini. Tafiti na chambuzi mbalimbali zimefanywa mwezi Septemba ambazo zitasaidia kwenye utekelezaji wa programu. Tafiti hizi ni pamoja na Utafiti wa Usawa wa Kijinsia, Ulemavu na Ujumuishi (GEDI), tathmini ya mifumo ya kuripoti matukio ya usalama shulemi, utafiti wa usimamizi na uongozi bora wa shule, utafiti wa uendeshaji wa Ushirikiano wa Walimu na Wazazi (UWW), uchunguzi wa Mfumo wa Taarifa za Shule (SIS), na uchunguzi wa wa Mfumo wa Usimamizi wa Taarifa wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC-MIS), na tathmini za uwezo kwa wafanyakazi wa sekta ya elimu katika ngazi za chini na kitaifa. Kwa ujumla, tafiti hizi zitasaidia katika kutengeneza muundo wa programu. Mpango wa tathmini ya awali utatekelezwa katika robo ya mwisho ya mwaka.

| Matarajio yajayo |
| --- |
| Shughuli zilizopangwa kutekelezwa mwezi Oktoba |
| Kupanga na kusaidia kujenga uelewa wa EP4R II katika Halmashauri na uandaaji wa mipango kazi |
| Kufanya mapitio ya Mkakati wa Kuajiri Walimu wa Shule za Msingi |
| Kuanza kutekeleza shughuli za Mbinu ya Kutafuta Ufumbuzi wa ndani wa tatizo na kufanyia majaribio (PDIA) na timu za utekelezaji katika wilaya tisa za kuanzia |
| Kuanza utekelezaji wa Mpango wa Kumuandaa Mtoto Kuanza Shule mkoa wa Pwani |
| Kukamilisha video za kusaidia kuendesha mafunzo ya Endelevu ya Waalimu kazini na kufanya mapitio ya mafunzo yaliyoendeshwa mwezi Septemba |
| Mafunzo ya Maafisa Habari wa Kitaifa, Mikoa na Halmashauri kwa mikoa ya Rukwa, Kigoma na Katavi |
| Kufanya tathmini ya Vituo vya Utambuzi na Upimaji wa Ulemavu(ESRAC) ili kubaini uwezo na kazi zao |
| Kukamilisha ripoti ya mbinu za kuripoti masuala ya usalama katika ngazi ya shule |
| Kubainisha mbinu fanisi za Uongozi na Usimamizi Bora (Halmashauri ya Mji wa Kasulu na Halmashauri ya Wilaya ya Uvinza) |

Shule Bora ni program ya kusaidia elimu inayoongozwa na serikali, na kufadhiliwa na UK aid. Inasaidia mchakato wa utekelezaji wa kitaifa wa Mpango wa Elimu wa Lipa Kulingana na Matokeo II (EPforR II) na pia inatekeleza kazi zake katika mikoa tisa ya Tanzania kutoa msaada wa kiutalamu chini ya Cambridge Education kwa kushirikiana na Mashirika ya ADD International, International Rescue Committee, na Plan International. Kwa maelezo zaidi tembelea **www.camb-ed.com au** wasiliana nasi kwa barua pepe kupitia **CETanzania@camb-ed.com**, au kwa simu kwa namba **+255 759 957880**

Funded by UK aid from the British Government, Shule Bora is a new national education programme that seeks to improve the quality, inclusiveness, and safety of learning for girls and boys in government schools in Tanzania.